

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA

Mawasiliano:

Simu: 0272-970677

Nukushi: 027-2970678

Barua pepe:

ded@sihadc.go.tz

Tovuti: www.sihadc.go.tz

Kumb. Na. SDC/T.20/41/07



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji
5 BR-Sanya Juu-Elerai
S.L.P 129,
25482 SIHA.

Tarehe: 28/12/2022

TANGAZO KWA UMMA

WALIOLIMA MAENEO YA HALMASHAURI BILA KULIPIA KWA MSIMU WA VULI 2022

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha-Kilimanjaro anawatangazia Wananchi/Watu wote waliolima msimu wa vuli 2022 maeneo yanayomilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Siha bila kulipia wafike Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji na kulipia kulingana na ukubwa wa maeneo waliyolima kabla ya tarehe 1/1/2023.

Wale wote watakaoshindwa kulipia maeneo waliyolima msimu huu wa vuli 2022, baada ya tarehe 01/01/2023 Halmashauri ya Wilaya ya Siha itayataifisha na kuyamiliki mazao yote yatakayokuwa shambani na hakuna mtu yeyote ataruhusiwa kuingia katika maeneo yote ambayo hayajalipiwa fedha za ukodishwaji wa mashamba.

NB. Fika Mapema na kulipia fedha kulingana na ukubwa wa eneo ulilolima kabla hatua kali za Kisheria hazijachukuliwa dhidi yako ikiwa ni pamoja na kupoteza mazao yaliyo shambani na kufikishwa katika vyombo vya Kisheria

Imetolewa na

Mangal U.E
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA

MKURUGENZI MTENDAJI (W,
SIHA